# TUNATEKELEZA JULAI, 2018

Na: Dkt. Hassan Abbasi, Msemaji Mkuu wa Serikali,

DODOMA, 25 JULAI, 2018

# UTANGULIZI

- Mkutano huu ni mwendelezo wa mikutano ya kila mwezi kati ya Msemaji Mkuu wa Serikali na wanahabari kwa lengo la kutoa mrejesho kwa umma, kupitia wanahabari, kuhusu kinachoendelea katika utekelezaji wa ahadi za Serikali.

- Nawapongeza na kuwashukuru wanahabari kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa Serikali katika Mwaka wa Fedha 2017/18, katika kusaidia kuhabarisha umma masuala mbalimbali ya utekelezaji wa shughuli za Serikali.

# UTANGULIZI

- Hata hivyo nitumie fursa hii kuwasisitiza wanahabari kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Habari na. 12, 2016 vyombo vya habari vinapaswa kutekeleza kazi zao kwa mujibu wa maadili ya kiwango cha juu sana;

- Tunashuhudia kuwepo kwa vitendo vya ukiukwaji wa maadili ya taaluma kwani pale Serikali itakapochukua hatua tusilaumiane;

- Aidha niwakumbushe wamiliki wa magazeti kuhuisha leseni zao za mwaka huu;

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA

- Hadi Machi 2017, pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 7.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2016. Ukuaji huu ulitokana na utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo na kimarika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi.

- Kilimo kutoka Asilimia 2.1 hadi 3.6;
- Mawasiliano Kutoka Asilimia 13.0 hadi 14.7;
- Madini kutoka Asilimia 11.5 hadi 17.7;
- Ujenzi Kutoka Asilimia 13.0 hadi 14.1;

# HALI YA UCHUMI WA TAIFA

- Maji Kutoka Asilimia 4.3 hadi 16.7

- Uchukuzi kutoka Asilimia 11.8 hadi 16.6
- Elimu kutoka Asilimia 8.1 hadi 8.5;
- Afya kutoka Asilimia 5.2 hadi 5.9.

# Makusanyo ya Kodi Yaongezeka

- Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilifanikiwa kukusanya Jumla ya Shilingi Trilioni 15.5 kuanzia Julai 2017 hadi Juni, 2018 ikilinganishwa na Shilingi Trilioni 14.4 ambazo zilikusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa Fedha 2016/17, kiasi hiki ni sawa na ukuaji wa Asilimia 7.5;

- Kwa niaba ya Serikali niwapongeze watendaji wote waliosimamia hili na wananchi waliolipa kodi na tuendelee na mshikamano huu huu.

# Makampuni Yaanza Kulipa Gawio na Mapato kwa Serikali

- Kutokana na utendaji makini wa Rais Magufuli na Serikali ya Awamu ya Tano kwa ujumla hata mashirika ambayo yalikuwa hayatoi gawio kwa Serikali sasa yanatoa:

- Juzi mmesikia zaidi ya TZS Bilioni 700 zimekusanywa kama gawio na mgawo wa asilimia 15 kutoka taasisi na mashirika ya umma na binafsi 43 na taarifa za sasa ni kuwa fedha hizi zitaongezeka hadi zaidi ya Bilioni 800 ikiwa ni baada ya taasisi nyingine kuhamasika na hii ni ongezeko la asilimia zaidi ya 500;

# UTEKELEZAJI KATIKA SEKTA MUHIMU KWA WANANCHI

# USAFIRI WA ANGA….TUMETIMIZA NDOTO

1. Serikali imetimiza ndoto ya kuendelea kulifufua Shirika la Ndege kwa kuleta Boeing 878 Dreamliner, Ndege nyingine 2 za C Series zinakuja Novemba na Boeing nyingine 1 itawasili Januari, 2020

2. Manufaa ya ndege hizi yameanza kuonekana ambapo zinasaidia wananchi wengi kusafiri kwa haraka na kufanyabiashara zao kwa haraka. Tangu tulete ndege hizi abiria wa ATCL waliongezeka HADI KUFIKIA 107,207 katika mwaka 2016/17 kutoka 49,173 mwaka 2015/16, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 118.

# UTEKELEZAJI WA SEKTA MUHIMU….







# HUDUMA ZA MAJI ZAENDELEA KUIMARISHWA

## ii.Huduma ya Maji Vijijini

Mwaka 2017, Serikali iliendelea kutekeleza miradi ya maji vijijini kupitia programu ya kuendeleza sekta ya maji kwa lengo la kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji vijijini, hadi kufikia Machi, 2017, ujenzi wa miundombinu ya **miradi 1,493** ulikamilika na **miradi 366** ujenzi wake unaendelea kutekelezwa sehemu mbalimbali nchini.

# UTEKELEZAJI WA SEKTA MUHIMU….



# UJENZI WA BARABARA UNAENDELEA NCHI NZIMA



# UJENZI WA BARABARA UNAENDELEA

Mwaka 2017, barabara kuu, barabara za mikoa na barabara za wilaya za kiwango cha lami na changarawe zilikuwa na urefu wa kilometa 32, 170 ikilinganishwa na kilometa 30,265 kwa mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 6.3;

Serikali pia iliunda wakala maalum wa kusimamia barabara za vijijini na miji midogo TARURA ambao wameshaanza kazi na unasogeza zaidi huduma vijijini.

# UZALISHAJI WA UMEME WAENDELEA…

Serikali inaendelea kukamilisha miradi mbalimbali ya umeme nchini: K1-extension ambako tayari mitambo imeanza kufungwa kutengeneza megawati 185;

Mtambo wa K-II ulitarajiwa kutengeneza megawati 240 sasa mvuko utasaidia kuzalisha megawati 40 zaidi hivyo zitakuwa megawati 280 na tayari takribani megawati 208.02 zimeshaingia katika gridi na mradi utakamilika Septemba mwaka huu;

Mradi ujao mkubwa ni Stiglers wa megawati 2,100 na utekelezaji wake utaanza mwaka huu wa fedha

# Mtambo wa megawati 40.2 unaotumia mvuke wa gesi kuzalisha umeme Kinyerezi-II



# UAMUZI WA KUHAMIA DODOMA

Serikali imeendelea kutekeleza agizo la kuhamia Dodoma ambapo takribani watumishi 6,400:

i. **Awamu ya Kwanza:** Awamu ya kwanza, watumishi 1,789 walihamia Dodoma;

ii. **Awamu ya Pili:** Kati ya Novemba, 2017 hadi Machi, 2018 watumishi 2,040 walihamia Dodoma.

iii. **Awamu ya Tatu:** Kati ya Mwezi Machi na Juni, 2018 watumishi 2600 wamehamia Dodoma

# ASANTENI SANA

**Imetolewa na:** Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Hassan Abbasi